

Usawiri wa Nduni za Shujaa katika Kisakale cha Munyigumba wa Jamii ya Wahehe

Aneth W. Kasebele¹

Ikisiri

Makala hii inachunguza usawiri wa nduni za shujaa katika Kisakale cha Munyigumba wa jamii ya Wahehe. Watafiti wa masuala ya nduni za shujaa wa Kiafrika wanaeleza kuwa kila jamii ina nduni zake za shujaa zinazotegemea mtazamo, falsafa na utamaduni wa jamii husika. Hivyo, si rahisi kwa jamii zisizo na uhusiano wa karibu kuwa na nduni za shujaa zinazolandana katika hali zote. Kuwapo kwa mitazamo na tamaduni tofautitofauti kunasababisha sifa za shujaa wa jamii moja kuwa tofauti na za shujaa anayepatikana katika jamii nyingine. Hivyo, kilichofanyika katika makala hii ni kubainisha nduni za shujaa wa jamii ya Wahehe ili kufahamu nduni zake. Makala hii imeongozwa na mawazo ya Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika kwa kuwa shujaa anayechunguzwa anatoka katika jamii za kijadi za Kiafrika. Data za makala hii zimekusanywa kwa njia ya usaili na uchambuzi matini kutoka katika vijiji vya Kalenga na Rungemba, Mkoani Iringa. Matokeo ya utafiti wa makala hii yameonesha kuwa shujaa wa jamii ya Wahehe ana nduni mbalimbali zilizohititika kupitia Kisakale cha Munyigumba. Aidha, imethibitika kuwa, jamii mbalimbali za Kiafrika zina mfanano mkubwa unaosababisha hata mashujaa wake kuwa na nduni zinazofanana kwa kiasi kikubwa.

1.0 Utangulizi

Wahehe ni jamii ya Kiafrika inayopatikana katika mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya. Hata hivyo, watafiti mbalimbali wanathibitisha kuwa idadi kubwa ya Wahehe inapatikana katika Mkoa wa Iringa na hasa katika kata za Malangali, Kinyanambo, Tanangozi, Rungemba, Luhota, Kalenga, Isole na Image, kwa kutaja baadhi (Kapinga, 2013; Msigala, 2015; Madumulla, 2017). Jamii ya Wahehe inatajwa kuwa na watawala mbalimbali na ni miongoni mwa jamii za Kiafrika zinazoelezwa kuwa zilikuwa na viongozi imara. Miongoni mwa viongozi waliotawala katika jamii ya Wahehe wamekuwa wakielezwa katika kazi mbalimbali za fasihi za zisizo za kifasihi kuhusu jamii hiyo. Kwa mfano, tamthiliya ya *Mukwava wa Uhehe* (Mulokozi, 1988) inasawiri maisha ya

¹ Mhadhiri, Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Tanzania. Barua pepe: aneth.kasebele@muce.ac.tz

Mukwavinyika tangu enzi za utawala wa baba yake Munyigumba mpaka kwa utawala wa Sapi. Pia, Mulokozi (1996, 2013 na 2018) anawaelezea watawala wa jamii ya Wahehe katika riwaya zake za *Moto wa Mianzi*, *Ngome ya Mianzi* na *Ngoma ya Mianzi*. Watawala anaowataja ni pamoja na Mukwavinyika na Sapi. Hii ni ithibati kuwa jamii ya Wahehe imekuwa na watawala wengi katika historia ya kuwapo kwake, ambao pia wengine walikuwa mashujaa. Aidha, Ngassapa (2011) anasimulia kuhusu *Mukwavinyika na Kabila Lake la Wahehe* na kutaja viongozi waliotawala katika jamii ya Wahehe ambao ni Mwamuyinga, Maliga, Mudegela, Kilonge, Munyigumba, Mwambambe, Mukwavinyika, Sapi na Adamu.

Katika makala hii, kwa hiyo, tumetafiti usawiri wa nduni za shujaa katika Kisakale cha Munyigumba wa jamii ya Wahehe. Imezoeleka kwa watafiti wengi kuwa mashujaa wanachambuliwa kwa kutumia utanzu wa ushairi (simulizi) katika kipera cha utendi. Hili, zaidi ya mengine, limesababisha hata mashujaa hao kujulikana kuwa ni mashujaa wa kiutendi. Pia, kumekuwa na tafiti chache kuhusu uchambuzi wa mashujaa wa Kiafrika kwa kutumia utanzu wa masimulizi kama visakale. Sababu ya kuteua visakale ni kuwa kipera hiki husimulia masimulizi ya kimapokeo kuhusu watawala, wahenga au mashujaa wa jamii kwa kuchanganya chuku na historia halisi. Hivyo basi, visakale, mbali na kutumia chuku, vinahifadhi historia halisi ya shujaa husika na jamii yake, kiasi kwamba wanajamii huziamini kuwa ni hadithi zihusuzo matukio ya kweli yaliyopata kutokea katika jamii. Katika jamii za Kiafrika, kuna masimulizi mengi ya mashujaa ambao habari zao zimechanganywa na visakale kama vile: “Sunjata”, “Shaka”, “Kinjeketile”, “Ng’wanamalundi”, “Mukwavinyika”, “Mirambo” na hata “Nyerere” (Mulokozi, 2017).

2.0 Muhtasari wa Kisakale cha Munyigumba

Kisakale cha Munyigumba kinamhusu Binini ambaye alikuwa ni mtoto wa mtawala wa nchi ya Ng’uluhe aitwaye Kilonge. Jina Binini katika jamii ya Wahehe halikupendelewa kutajwa kwa sababu linadhihirisha umbo lake la mwili hasa la mabega manene sana. Isivyo bahati, baada ya kumzaa mtoto huyo wa pili, mama yake Binini alifariki dunia. Baada ya mama yake kufariki dunia, Binini alienda kulelewa kwa mjomba wake, Mzee Mihwela, huko Luhota. Hata hivyo, baada ya miaka kadhaa kupita, mtawala Kilonge alifariki dunia na utawala ulibaki mikononi mwa kaka yake Binini aliyelitwa Ng’awonalupembe. Pia, huko Luhota baada ya mjomba wake kufariki dunia, utawala uliachwa kwa mtoto wake mkubwa wa kiume aitwaye Muyoveligombo. Kutokana na uchu wa madaraka na kutaka atawale yeye, kitendo cha Ng’awonalupembe na Muyoveligombo kuachiwa madaraka hakikumfurahisha Binini. Hivyo, alianza kufanya njama za kutwaa madaraka. Kwanza, alimuua kaka yake, Ng’awonalupembe. Vilevile, aliwadhulumu utawala watoto wa mjomba wake, Mzee Mihwela, ili kote atawale yeye. Aidha, aliziteka jamii za jirani na kuimarisha himaya yake. Hata alipoitwa ili arudi Ng’uluhe katika msiba wa kaka yake alikataa na badala yake alienda

kupigana vita na Wasangu. Katika vita hivyo, Binini alishinda kisha akarithi jina la mtawala wa Wasangu aliyeitwa Munyigumba, ndipo ukawa mwanzo wa Binini kuitwa Munyigumba. Baada ya ushindi alioupata kutoka kwa Wasangu, Munyigumba alirudi Ng'uluhe huku akiwa na mali nyingi na mamlaka ya kifalme na akaanza kutawala rasmi.

Katika kisakale hicho, inaelezwa kuwa utawala wa Munyigumba ulijaa ugomvi kutokana na kupigana vita mara kwa mara na majirani zake. Hata hivyo, Munyigumba alishinda vita vingi kutokana na msaada wa dawa za kivita alizokuwa anazitumia. Kwa mfano, siku moja, Wangoni walienda kumvamia Munyigumba nyumbani kwake ambapo kwa hofu ya kuuawa alitoroka na kwenda kujificha pangoni. Hata hivyo, Wangoni walimwona Munyigumba alikoenda kujificha, na hivyo, wakaenda kuliziba pango alilojificha ili afie humo. Hata hivyo, Mukwavinyika, mtoto wa Munyigumba, aliipuliza dawa ya kivita iliyofufua nguvu za dawa aliyokuwa nayo Munyigumba, na hivyo, kumwokoza Munyigumba.

Vilevile, katika kisakale hicho, imeelezwa kuwa Munyigumba ndiye mtawala pekee ambaye aliunganisha jamii moja ya Wahehe kutoka katika jamii ndogondogo. Pia, inaelezwa kuwa Munyigumba alikuwa mtawala mwenye nguvu na uhodari katika kutumia mishale na mikuki kupambana na maadui wake. Inaelezwa katika kisakale hicho kuwa, hakuna mtu aliyeweza kumshinda Munyigumba kwa kuwa alikuwa na jeshi lenye nguvu. Hata Wangoni, ambao kwa kipindi hicho ndio walikuwa wanasifika kuwa na jeshi imara na ufundi wa kivita, walishindwa kwa Munyigumba.

3.0 Nadharia na Mbinu za Utafiti

Sehemu hii imefafanua msingi wa kinadharia na mbinu za utafiti zilizotumika katika makala hii kama ifuatavyo:

3.1 Nadharia

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Mawazo ya nadharia hii yameasisiwa na Placide Tempels katika Karne ya 20 alipoandika kitabu chake cha *Bantu Philosophy* (1945). Baada ya kazi ya Tempels, kumekuwapo na watafiti mbalimbali walioshughulikia Ontolojia hii. Watafiti hao ni kama vile: Mbiti (1969), Kezilahabi (1985), Nicholas (2011), Chuachua (2016), Mulokozi (2017) na Mpalanzi (2019). Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika imejikita katika tajiriba ya Waafrika tangu kale katika mifumo ya kijamii na kiutawala, uzalishaji wa rasilimali na ugawaji wa rasilimali hizo.

Wafuasi wa Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika wameeleza misingi au mihimili mbalimbali ya nadharia hii. Mojawapo ya mihimili hiyo ni imani ya Waafrika kuwa kuna Mungu lakini katika darajia. Darajia hizo zinaanzia kwa Mungu, wahenga au mizimu, wazee, watu mashuhuri, watu, wanyama na mimea. Pia, wanaamini katika familia pana. Hii ina maana kwamba Waafrika huishi na hujitambulisha kwa kuwa na familia pana yenye kujumuisha watu waishio sasa,

wahenga waliofariki na watu ambao hawajazaliwa. Vilevile, Waafrika wanathamini sana uzazi kwa sababu wanaamini kuwa uzazi ndio njia ya uzima wa milele na ugumba ni laana. Sio hivyo tu, bali pia Waafrika wanaamini katika wahenga au mahoka ambao ni watu waliokufa zamani lakini bado wanakumbukwa na ni sehemu ya familia. Mbali na mihimili hiyo, Waafrika wanaamini pia katika sihiri. Kwa mujibu wa Mulokozi (2017), sihiri hujumisha nguvu za ziada ambazo mtu anazipata kutoka kwa mganga, ambazo humsaidia katika kufanikisha masuala mbalimbali. Aidha, Waafrika wana imani kwamba mtu ana uwezo wa kuongoza au kubadilisha majaliwa yake. Halikadhalika, Waafrika wanatambua na kuenzi uzalishaji mali kama msingi wa uhai, maisha, kaya na jamii. Mbali na hayo, mhimili mwingine wa Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika unaeleza kuwa, Waafrika wanaamini kuishi katika umoja, mshikamano na ukamilishano wa maumbile na vilivyomo. Hii ni baadhi ya mihimili ya Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika ambayo kwa namna moja ama nyingine imetusaidia katika uchambuzi wa data za makala hii kuhusu usawiri wa nduni za shujaa katika Kisakale cha Munyiigumba wa jamii ya Wahehe.

3.2 Mbinu za Utafiti

Data za utafiti huu zilipatikana uwandani mkoani Iringa, katika Kata ya Kalenga na Rungemba, Mkoa wa Iringa uliteuliwa kwa sababu ndio mkoa ambao jamii kubwa ya Wahehe inaishi. Pia, Kata ya Rungemba iliteuliwa kwa sababu ndipo panapoelezwa kuwa aliishi shujaa Munyiigumba. Vilevile, Kata ya Kalenga iliteuliwa kwa sababu kuna nyaraka mbalimbali zilizohifadhiwa zinazohusu maisha ya mashujaa wa jamii ya Wahehe katika Makumbusho ya Kalenga. Hivyo, katika kata hiyo, mtafiti alipata historia ya kina kuhusu shujaa Munyiigumba ambaye pia anarejelewa katika kisakale. Katika ukusanyaji wa data, mtafiti alitumia mbinu ya usaili na uchambuzi matini. Mbinu ya usaili ilitumika kwa sababu inahusisha ukusanyaji wa taarifa kwa kutumia mazungumzo baina ya mtafiti na watoa taarifa wake. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kukusanya data kuhusu Kisakale cha Munyiigumba. Aidha, mbinu ya uchambuzi matini iliteuliwa ili kukusanya data ambazo hazikuweza kukusanywa kwa kutumia njia ya usaili. Matini zilizochambuliwa ni zile zinazohusu historia ya jamii ya Wahehe, simulizi kuhusu mashujaa zisizokuwa za kifasihi na zile za kifasihi.

Katika uchambuzi wa data, mtafiti alianza kwa kunukuu masimulizi kuhusu Kisakale cha Munyiigumba. Kwa kufanya hivyo, mtafiti aliweka data za masimulizi katika maandishi. Hatua iliyofuata, mtafiti alibainisha data za utafiti huu kulingana na lengo la makala hii. Baada ya kubainisha data, hatua iliyofuata, mtafiti alichambua data kwa kuhusisha na mihimili ya Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Hatua ya mwisho, mtafiti alichambua na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Mkabala wa kitaamuli, unaolenga kuchambua na kuwasilisha data kwa njia ya maelezo, ndio uliotumika katika utafiti huu. Kwa kutumia mkabala huu,

uchambuzi na uwasilishaji wa data ulifanyika ili kuonesha usawiri wa nduni za shujaa katika Kisakale cha Munyigumba wa jamii ya Wahehe.

4.0 Usawiri wa Nduni za Shujaa katika Kisakale cha Munyigumba

Katika sehemu hii, tumefafanua jinsi nduni za shujaa zilivyosawiriwa katika Kisakale cha Munyigumba kama ifuatavyo:

4.1 Shujaa huwa na Nguvu za Kivita

Nduni ya kwanza ya shujaa inayosawiriwa katika Kisakale cha Munyigumba ni shujaa kuwa na nguvu za kivita. Watawala wa jamii ya Wahehe walikuwa wanaongoza mapigano ya kivita ambapo katika mapigano mengi, kwa kiasi kikubwa, walikuwa wanashinda. Katika jamii nyingi za Kiafrika mashujaa walipigana vita kwa lengo la kuzikomboa jamii zao kutoka katika mikono ya maadui au watu waliowatendea mabaya. Suala la watu waliotenda mabaya kuadhibiwa linaendana na Ontolojia ya Kiafrika inayobainisha kuwa mwisho wa ubaya ni aibu (Mulokozi, 2017). Hivyo basi, jamii za Kiafrika zilipigana vita ili kulipiza visasi au kutoa adhabu na maonyo kwa watu au jamii zilizowatendea mabaya.

Suala la shujaa kuwa na nguvu za kivita linabainika wazi katika Kisakale cha Munyigumba. Katika kisakale hicho, imeelezwa kwamba Binini alipigana vita na Wasangu, ambapo katika vita hivyo alishinda. Kutokana na nguvu nyingi za kivita alizokuwa nazo, aliwashinda Wasangu na kujibatiza jina la mtawala wao, Munyigumba, kuwa jina lake. Suala hilo linathibitika katika kisakale hicho inapoelezwa kuwa:

...Binini alipoarifiwa kuhusu msiba wa kaka yake na kutakiwa kwenda Ng'uluhe msibani, hakwenda. Alijisema “ameshakufa mbwa yule wacha wamfukie. Sasa Nimeshakuwa Mutwa. Ngoja kwanza nikapigane vita na Wasangu.” Katika mapigano hayo ya kivita, Binini alishinda kwa kumchinja kama kuku Chifu wa Wasangu aliyetitwa Munyigumba. Baada ya kupata ushindi ndipo Binini akajiita Munyigumba...

Maelezo haya yanatuonesha jinsi Munyigumba alivyopenda vita. Hapa tunaona Munyigumba kuwa, kutokana na kupenda vita, hakuthamini mazishi ya kaka yake. Hivyo, badala ya kwenda mazishini, yeye alikwenda vitani. Alipokuwa huko vitani, Munyigumba alishinda vita baada ya kuwashinda Wasangu.

4.2 Shujaa huwa na Nguvu za Sihiri

Nduni nyingine ya shujaa iliyosawiriwa katika Kisakale cha Munyigumba ni shujaa kuwa na nguvu za sihiri. Suala la shujaa kuwa na nguvu za sihiri limefungamana na imani ya jamii husika, ambapo katika jamii za Kiafrika, huaminika kuwa sihiri ni moja ya njia ya kutatua matatizo mbalimbali ya wanajamii (Mulokozi, 2017; Mpalanzi, 2019). Akifafanua mawazo haya ya

Kiontolojia ya Kiafrika, Mulokozi (2017) anaeleza kwamba Waafrika hutumia nguvu za sihiri kutatua matatizo mbalimbali yanayoonekana kukosa ufumbuzi wa kawaida wa kibinadamu.

Katika Kisakale cha Munyigumba, Shujaa huyo anatajwa kuwa alikuwa na nguvu nyingi za sihiri zilizomsaidia kushinda vita. Aidha, mbali na Munyigumba wa jamii ya Wahehe, watawala wengine wa Kiafrika wanaotajwa kutumia nguvu za sihiri ni pamoja na Sundiata na Malkia Nzinga Mbandi (Johnson, 1986; Ribeiro na wenzake, 2019). Kila Munyigumba alipokuwa na vita, alitumia dawa mbalimbali za kijadi za kivita zilizomwezesha kushinda vita hivyo. Katika zama za Munyigumba, Mwambambe, aliyekuwa askari wa Munyigumba alitumwa porini kuchukua dawa hizo kwa ajili ya kushinda vita. Suala la Munyigumba kutumia nguvu za sihiri kushinda vita limebainika katika kisakale chake kama ifuatavyo:

...Siku moja jeshi la Wangoni lilipenya Ubena likaingia Uhehe ili kumvamia Munyigumba. Wangoni hao walikuwa wamechachamaa kama moto uliochochewa kuni kavu kutokana na bangi waliyozoea kuivuta kabla ya mapigano. Hivyo, hawakuwa na hofu wala kujali maumivu, jeraha au kifo kama mawimbi ya mafuriko yasiyoweza kuzuiwa. Kwa sababu hiyo, Munyigumba hakuweza kuwapiga Wangoni akawa hana budi kukimbilia kwenye mapango ya Nyamulenge. Hata hivyo, Wangoni walimtafuta na kujua kuwa Munyigumba alijificha pangoni, wakamfuata na kuziba mle pangoni ili asiweze kutoka. Kwa bahati nzuri, huko nyuma, vikosi vya Munyigumba vilivyokuwa vinaongozwa na Mukwavinyika vilirejea. Mukwavinyika alikusanya vikosi vyake haraka na akachukua dawa ya kiutawala iliyoitwa "lihomelo" akafanya kama ambavyo alielekezwa na baba yake. Ghafla, walipokuwa pangoni Munyigumba alishangaa kuona dawa aliyokuwa nayo inaanza kufuka moshi na inageuka rangi na kuwa nyekundu. Kitendo cha dawa kugeuka rangi ilikuwa ni ishara kwamba watakombolewa. Dawa ilipobadilika rangi na kuwa nyekundu ilipata nguvu. Baada ya dawa yake kupata nguvu, Munyigumba akaenda kuimwaga kwenye jiwe ili ule moshi uwapate Wangoni. Wangoni walipoupata ule moshi walilala usingizi palepale. Munyigumba na wafuasi wake walipoona kuko kimya hapo hapo wakapata njia ya kutoka pangoni. Walipokuwa wanatoka pangoni Munyigumba aliwaambia wafuasi wake wasimpige risasi Mngoni yeyote wala kumkanyaga...

Maelezo haya yanadhihirisha jinsi shujaa Munyigumba alivyokuwa anatumia nguvu za kisihiri ambazo zilimsaidia kushinda vita. Kitendo cha Munyigumba kutoka salama pangoni kinaonesha jinsi sihiri yake ilivyokuwa na nguvu. Aidha, Malangalila (1987) anaeleza kuwa Munyigumba alikuwa anatumia dawa nyingi kwa ajili ya kujizindika. Zindiko lake kuu lilikuwa ni kwa wake zake aliokuwa

anawaoa. Malangalila anaeleza kuwa kila Munyigumba apofiwa na mke wake alikuwa anaoa harakaharaka ili asijulikane kama yeye ndiye mchinjaji.

4.3 Shujaa huwa na Nguvu za Kiakili

Mbali na nduni hizo, nduni nyingine ya shujaa wa Kiafrika inayosawiriwa katika Kisakale cha Munyigumba ni shujaa kuwa na nguvu za kiakili. Katika kisakale hicho imeelezwa kuwa Munyigumba alikuwa mjanja na mwenye akili nyingi tangu alipokuwa kijana mdogo wakati anaishi kwa mjomba wake, Mzee Mihwela, huko Luhota. Munyigumba alipokuwa anaishi huko Luhota alianza kutumia akili ili awe mtawala kwa kumfundisha ujeuri mtoto wa Mzee Mihwela aliyeitwa Mwengamagoha. Munyigumba alitumia akili kubaini kuwa Mwengamagoha atakuwa mrithi wa madaraka, hivyo, akawa karibu naye ili aweze kumpindua na kutwaa madaraka. Hoja hii imenukuliwa kama ilivyoelezwa katika kisakale cha Munyigumba.

...Siku moja Binini alikuwa anamchochea mtoto wa mjomba wake aitwaye Mwengamagoha afanye ujeuri kwa baba yake ili Mwengamagoha apate kuwa mtawala. Lengo la Binini lilikuwa endapo Mwengamagoha atatawala basi itakuwa rahisi kwake kumnyang'anya madaraka. Hata hivyo, ujanja wa Binini ulikuja kugunduliwa na mjomba wake kuwa ujeuri anaoufanya Mwengamagoha unachochea na Binini...

Hapa inabainika kuwa Munyigumba alikuwa anatomia akili na ujanja kwa kumchochea Mwengamagoha afanye ujeuri ili apate kurithi madaraka ya baba yake. Kutokana na hayo, ingekuwa rahisi sana kwa Munyigumba kumpora madaraka Mwengamagoha kwa sababu Munyigumba alikuwa anafahamu kuwa Mwengamagoha hana nguvu za kupambana naye. Matumizi ya mbinu hii yanaonesha wazi kuwa Munyigumba alikuwa mjanja na ana akili nyingi zilizomwezesha kuchambua mambo na kupanga mikakati ya kuwa mtawala.

4.4 Shujaa huwa na Nguvu za Kimwili

Imebainika pia kuwa nduni nyingine ya shujaa inayosawiriwa katika Kisakale cha Munyigumba ni shujaa kuwa na nguvu za kimwili. Shujaa wa jamii ya Kihehe anapaswa kuwa na nguvu za kimwili zitakazomuwezesha kutenda masuala mbalimbali yanayohitaji nguvu nyingi. Masuala hayo ni pamoja na kufanya shughuli za kilimo, kupigana vita na kuteka maadui. Suala la wanajamii kuwa na nguvu za kimwili ni suala la Kiontolojia ya Kiafrika. Katika Ontolojia ya Kiafrika, kuwa na nguvu za kimwili ni jambo muhimu na mtu mvivu na asiye na nguvu alionekana kuwa mtu asiyekubalika katika jamii. Katika jamii mbalimbali za Waafrika, ikiwa ni pamoja na jamii ya Wahehe, mtu asiyekuwa na nguvu na mvivu hukejeliwa. Hata semi mbalimbali huonesha umuhimu wa nguvu. Mfano wa semi hizo ni: asiyefanya kazi na asile, kazi ndiyo kipimo cha utu, mvivu hana rafiki, mwisho wa mvivu ni njaa (Samwel, 2015). Hivyo, suala la kuwa na nguvu

za kimwili ni mojawapo ya masuala muhimu katika jamii za Waafrika. Aidha, shujaa kuwa na nguvu hizo kulitokana na shujaa husika kuwa na uzoefu katika masuala mbalimbali yatumiayo nguvu na pia mwili wake kuwa mkubwa.

Katika Kisakale cha Munyigumba, suala la shujaa kuwa na nguvu za kimwili limesawiriwa, ambapo imeelezwa kwamba Munyigumba alikuwa na nguvu nyingi zilizomwezesha kurusha mkuki na ukaenda juu sana kwa kasi kubwa. Kurusha mkuki na kwenda mbali kunategemea sana nguvu za mrushaji. Mtu mwenye nguvu kidogo akirusha mkuki hautakwenda mbali ikilinganishwa na kama mkuki huo utarushwa na mtu mwenye nguvu nyingi. Hivyo, kuweza kurusha mkuki na ukaenda mbali na kwa kasi kubwa, kunaonesha jinsi Munyigumba alivyokuwa na nguvu nyingi za kimwili. Katika Kisakale cha Munyigumba, suala hili la kuwa na nguvu nyingi za kimwili zilizosababisha aweze kurusha mikuki kwa kasi kubwa na kwa umbali mrefu linabainika katika nukuu ifuatayo:

...Munyigumba alipewa jina la Mugohang'amwa kwa sababu alikuwa na uwezo wa ajabu wa kurusha mkuki kwa nguvu...

Suala lililo wazi linalobainika hapa ni kuwa Munyigumba alikuwa na nguvu za kimwili kwa sababu alikuwa na uwezo wa kurusha mikuki iendayo juu kwa kasi sana. Nguvu hizo za kimwili zilimsaidia sana shujaa husika katika harakati zake za kuwa shujaa kwani zilimwezesha kuwa na nguvu za kimwili na kushinda vita mbalimbali alivyopigana.

4.5 Shujaa huwa na Umbo Kubwa na la Kutisha

Vilevile, imebainika kuwa nduni nyingine ya shujaa inayosawiriwa katika Kisakale cha Munyigumba ni shujaa kuwa na umbo kubwa. Suala hili la shujaa kuwa na umbo kubwa linahusishwa na mhimili wa Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika kuwa, Waafrika wanauona uzuri wa kitu ukiwa katika umbo hasa la duara (Mulokozi, 2017; Mpalanzi, 2019). Hivyo, kama mtu au kitu kikiwa na umbo jingine nje ya duara kinaonekana ni kibaya kwa Mwafrika. Katika jamii ya Wahehe ukubwa wa umbo ulimaanisha wingi wa nguvu na utisho kwa maadui. Usawiri wa shujaa kama mtu mwenye umbo kubwa unabainika katika Kisakale cha Munyigumba. Katika kisakale hicho, shujaa Munyigumba anaeleza kuwa na umbo lenye mabega manene sana ambalo ni tofauti na binadamu wa kawaida. Kinachobainika hapa ni kuwa Munyigumba, kutokana na ukubwa wake, hakuwa na uzuri wowote wa sura. Umbo hili kubwa lilimfanya awe mwenye kuogofya na kutisha kwa watu. Suala hili, limeelezwa katika kisakale hicho kama ifuatavyo:

...Mutwa Kilonge alikuwa na watoto wawili, wa kwanza aliitwa Ngawonalupembe na wa pili aliitwa Binini. Jina Binini alipewa kutokana na maumbile yake, ambapo alikuwa na mabega manene kuzidi masikio ya tembo na hivyo hakuwa na mwonekano mzuri...

Suala hili linadhihirisha kuwa hapo awali Munyigumba aliitwa Binini kutokana na umbo lake lenye mabega manene lililomfanya asiwe na mvuto kwa sababu

halikuwa umbo la duara kama Waafrika wanavyouona uzuri uweje. Nduni hii ya kuwa na umbo kubwa ilimsaidia Binini kuwa shujaa kutokana na kuogopwa na watu kwa kuwa na mwonekano wa kutisha.

4.6 Shujaa huwa na Jina la Heshima

Kwa kawaida, imezoeleka kuwa binadamu yeyote anapozaliwa hupewa jina. Samwel (2015) anabainisha kuwa utoaji wa majina katika jamii za jadi za Kiafrika ulizingatia sana nduni alizonazo mtu na pindi nduni hizo zilipobadilika, majina nayo yalibadilishwa. Katika utafiti huu, imebainika kuwa katika jamii ya Wahehe, mashujaa walipewa majina ya heshima yanayosawiri matendo yao. Majina hayo ya heshima, yalijulikana zaidi ya majina yao halisi waliyopewa na wazazi wao wakati wa kuzaliwa. Suala hili linabainika katika Kisakale cha Munyigumba, ambapo shujaa Munyigumba anarithi jina la chifu wa Wasangu aliyeitwa Munyigumba. Katika kisakale hicho, imeelezwa kuwa Munyigumba alirithi jina la Chifu wa Wasangu baada ya kumuua kwa ajili ya ukumbusho wake. Hivyo, jina hilo lilionesha nguvu kubwa aliyonayo Binini kiasi cha kuweza kumshinda Chifu wa Wasangu, Munyigumba. Hoja hii ya Waafrika kurithi majina imeelezwa na wananadharia wa Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika kama vile Tempels (1945) ambaye anasema kwamba Waafrika wanaamini kifo sio mwisho wa uhai bali ni mwanzo wa kuishi maisha mengine. Tempels anaeleza kuwa mtindo wa Waafrika wa kurithi majina ya watu waliofariki ni mojawapo ya uthibitisho kwamba mtu aliyekufa bado anaendelea kuishi. Hivyo, Munyigumba alirithi jina la kiongozi wa Wasangu ambaye alikuwa ni mtawala mwema na mwenye nguvu na jeshi kubwa. Kurithi huko kwa jina la Munyigumba, kulimaanisha kuwa Binini ni mwema na mwenye nguvu kijeshi; kulimaanisha Munyigumba anaishi ndani ya Binini. Suala hili linabainika katika maelezo yafuatayo kutoka katika kisakale husika.

...Katika mapigano hayo ya kivita, Binini alishinda kwa kumchinja kama kuku Chifu wa Wasangu aliyeitwa Munyigumba. Baada ya kupata ushindi ndipo Binini akajiita Munyigumba. Basi Munyigumba alirudi Ng'uluhe na mamlaka ya kifalme, ambapo nchi nzima ilitetemeka mfalme kaingia na akaanza kutawala rasmi katika nchi ya Ng'uluhe...

Maelezo haya yanathibitisha kuwa mara baada ya kupata ushindi kutoka katika vita na Wasangu, Munyigumba anapata jina jipya. Jina hili ndilo lililovuma na kufahamika sehemu mbalimbali zaidi ya jina lake alilopewa na wazazi wake baada ya kuzaliwa, Binini.

4.7 Shujaa Hulipiza Kisasi

Kulingana na Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika, kila ubaya aufanyao mtu una malipo, ambayo pia ni mabaya. Ni kutokana na hilo, wanajamii wamekuwa wakijitahidi sana kutenda mema kwa hofu ya kulipwa mabaya kutokana na ubaya wao (Samwel, 2015). Samwel (2015) anabainisha kuwa kutokana na umuhimu wa

falsafa hii katika jamii za Kiafrika, hata semi mbalimbali zilisawiri dhana hiyo, ambapo kuna semi kama vile: “mwisho wa ubaya aibu,” “wema hauozi,” “tenda wema nenda zako usingoje shukurani,” “malipo ni hapa hapa duniani ahera ni kwenda kuhesabiwa,” na nyinginezo. Semi hizi zinawasisitiza wanajamii kutenda mema na kuacha kutenda mabaya kwani kila baya lazima litalipwa kwa ubaya pia, ila wema huwa na malipo mema. Kutokana na hilo, katika jamii za Kiafrika, ni suala linalokubalika kwa mtu aliyekosewa kulipiza kisasi cha makosa aliyotendewa. Kutokana na hilo, mashujaa katika jamii mbalimbali za Kiafrika wamebainika kulipiza kisasi kwa makosa waliyotendewa.

Katika jamii ya Wahehe, suala la shujaa kulipiza kisasi linajitokeza pia. Kwa mfano, katika Kisakale cha Munyigumba, inabainika kuwa Munyigumba alilipiza kisasi kwa binamu yake Musambila. Munyigumba alilipiza kisasi kwa Musambila kwa sababu alimnyima askari wa kwenda nao vitani alipokuwa anataka kwenda kupigana vita na Wasangu. Kitendo cha Munyigumba kunyimwa askari kilimuudhi sana kiasi kwamba aliamua kulipiza kisasi kwa Musambila. Suala hili linaelezwa katika kisakale hicho kama ifuatavyo:

...Katika safari yake ya kurudi Ngu'luhe, Munyigumba alipita Mufindi kwa binamu yake Musambila. Munyigumba alipokewa kwa shangwe na sherehe za ngoma na kuandaliwa karamu. Ghafla, katikati ya michezo ya ngoma Munyigumba alisimama na kuruka juu karibia na kushika mbingu akamfuma binamu yake kwa mkuki aliourusha kwa kasi ya ajabu vuuuuuuuuuu! Mkuki aliourusha Muiyigumba ulisafiri safari ya masafa marefu ukaenda kutua kwa Musambila, hapohapo Musambila akakata roho kama kuku mwenye kideri...

Kisasi cha Munyigumba kwa Musambila kinatokana na kinyongo cha Munyigumba kunyimwa askari wa kivita. Hivyo, ingawa Munyigumba alishinda vita na kurudi kwake, alijiona ana wajibu wa kulipiza kisasi kwa Musambila kwa kile alichokitafsiri kuwa kosa alilomfanyia. Hivyo, alipanga safari ya kisasi aliyosingizia ni ya kwenda kumsalimia mjomba wake Musambila.

4.8 Shujaa Hufuata Kani ya Nasaba ya Kikeni

Nduni nyingine ya shujaa wa Kiafrika iliyobainika kusawiriwa katika Kisakale cha Munyigumba ni shujaa kufuata kani ya nasaba ya kikeni. Katika kisakale hicho, imebainika kuwa shujaa Munyigumba anafuata kani ya nasaba ya kikeni. Kinachoonekana katika kisakale hiki ni kuwa chimbuko la ukoo wa Munyigumba ni mtawala aliyeitwa Mwamuyinga. Mwamuyinga alirithi utawala wa jamii hii baada ya kufariki babu yake mzaa mama aitwaye Mududa. Mududa alimpa madaraka Mwamuyinga kwa sababu hakuwa na mtoto wa kiume ambaye angeweza kumrithisha madaraka hayo (Malangalila, 1987; Ngassapa, 2011). Hivyo, Mwamuyinga alipotawala katika jamii hii, alitawala katika jamii ya ukoo wa upande wa mama yake. Kutokana na hayo, kizazi cha Munyigumba mpaka kwa Mukwavinyika ni mwendelezo wa watawala wanaotawala katika ukoo wa

upande wa mama. Suala la kuwapo kwa kani kike na kiume linafungamana na Ontolojia ya Kiafrika kama inavyobainika kwa Mulokozi (2017). Mulokozi anabainisha kuwa shujaa huweza kutokana na kani kike au kiume. Suala la usawiri wa shujaa kutokana na kani kike limefafanuliwa na mmoja wa watoataarifa wetu kutoka Kijiji cha Rungemba kuwa:

...Asili ya ukoo wetu imetokana na mtu aliyeitwa Mufwimi aliyetokea Ethiopia akaingia Ng'uluhe kwa kupitia njia ya Dabaga. Mufwimi alipofika Ng'uluhe alipokelewa na Chifu Mwamududa. Mufwimi alipokuwa anaishi kwa Chifu Mwamududa alianzisha mahusiano ya siri ya kindoa na binti wa Mwamududa mpaka binti huyo akapata mimba. Baada ya muda kidogo kupita, Mufwimi aliambiwa na binti wa Chifu Mududa kuwa ameshika mimba. Mufwimi aliposikia hivyo aliamua kutoroka na kukimbilia Itamba ambako aliawa na nyati. Binti wa Mududa alipojifungua mtoto wa kiume alimuita Mwamuyinga jina ambalo aliagizwa na Mufwimi ampatie mtoto atakayezaliwa. Mtoto huyo aliyezaliwa alilelewa na babu yake Mwamududa na Mwamududa kwa kuwa hakuwa na mtoto wa kiume aliagiza kuwa atakapofariki utawala utabaki mikononi mwa Mwamuyinga...

Munyigumba pamoja na mtoto wake Mukwavinyika wanatawala katika utawala wa ukoo wa upande wa mama yao na si wa baba yao. Vilevile, katika Kisakale cha Munyigumba tunaona suala la shujaa kutokana na kani ya nasaba ya kikeneni. Katika kisakale hicho, tunaona kuwa Munyigumba anatawala pia Luhota katika himaya ya mjomba wake, ambaye kimsingi ni kaka wa mama yake. Hivyo, ushujaa wa Munyigumba unaotokana na kuwa na maeneo mengi ya utawala unatokana na kani ya kikeneni. Katika kisakale husika inaelezwa kuwa:

...Siku moja Munyigumba alipata taarifa ya kifo cha mjomba wake, Mzee Mihwela, huko Luhota. Kutokana na mahusiano yao mazuri, watoto wa Mzee Mihwela, ambao ni Mwengamagoha na Muyoveligombo, waliamua kumgawia Munyigumba sehemu ya mali kwa kuwa walilelewa naye pamoja. Baada ya Munyigumba kuambiwa atapewa sehemu ya mali alikataa na akadai sehemu ya nchi...

Kwa ujumla, imebainika kuwa shujaa wa jamii ya Kihehe anafuata kani ya nasaba ya kikeneni kwa sababu ametawala katika himaya ya ukoo wa mama na si wa baba. Hii inathibitisha kuwa mama ni mtu wa thamani katika jamii ya Wahehe kwa sababu mama amekuwa ndio nguzo kuu ya utawala wa mashujaa wa jamii hii.

4.9 Shujaa Hujiambia Jaala yake

Nduni nyingine ya shujaa inavyobainika kusawiriwa katika Kisakale cha Munyigumba ni shujaa kujiambia jaala yake. Suala la shujaa kujiambia jaala yake linaendana na mawazo ya Ontolojia ya Kiafrika kuwa Waafrika huamini kuwa shujaa anaweza kuifuata au kuiumba jaala yake (Nicholaus, 2011; Mulokozi, 2017). Katika Kisakale cha Munyigumba, inasawiriwa kuwa Munyigumba, tangu

akiwa mtoto, alikuwa na tamaa ya kutaka kuwa mtawala, jambo ambalo kwa dhahiri lisingewezekana kwa kuwa alikuwa na kaka zake ambao kwa mila na desturi za jamii hiyo ndio walitarajiwa kuwa warithi wa utawala. Aidha, hata Munyigumba alipokuwa analelewa kwa mjomba wake huko Luhota, alianza kutamani kuwa mtawala wakati katika hali ya kawaida isingewezekana yeye kurithi utawala wa mjomba wake. Juhudi na tamaa ya Munyigumba kuwa mtawala ndizo zilizomwezesha kuwa mtawala wa maeneo yote mawili aliyoyatamani. Hivyo, Munyigumba alijiambia jaala yake kutokana na juhudi zake na tamaa aliyokuwa nayo na si kutokana na majaliwa ya Mungu. Maelezo yafuatayo kutoka katika kisakale hicho yanabainisha hili:

...Baada ya msiba kuisha kaulimbiu ikapigwa “wana Ng’uluhe wana Nguluhe! Kutokana na msiba uliotufika kwa sasa Mutwa ni Ngawonalupembe.” Habari za Ngawonalupembe kutawazwa kuwa Mutwa zilimfikia Binini na kumkasirisha sana maana alitamani yeye ndiwe awe Mutwa hata hivyo alijikaza kisabuni bila kuonesha chuki yoyote. Siku zikaenda zikaenda lakini hatimaye uvumilivu ulimshinda. Binini akapanga njama na kufanikwa kumuua kaka yake. Loooh! Maskini Ngawonalupembe aliuawa na ndugu yake wa damu hata kabla ya kuufaidi utawala alioachiwa na baba yake...

Kwa ujumla imebainika kuwa Munyigumba alikuwa na tamaa ya kutaka kutawala yeye ilhali utamaduni wa jamii ulikuwa haumruhusu yeye kutawala kwa kipindi hicho. Hata hivyo, Munyigumba alitumia nguvu zake ambazo zilimwezesha kupata madaraka. Munyigumba hakuishia hapo bali pia alitaka kutawala mpaka katika utawala wa mjomba wake jambo ambalo katika hali ya kawaida lilikuwa haliwezekani, lakini kwa jitihada zake liliwezekana.

4.10 Shujaa Husafiri na kwenda Kuishi Uhamishoni

Pia, katika Kisakale cha Munyigumba nduni ya shujaa kusafiri na kwenda kuishi uhamishoni imejitokeza. Kwa mfano, Senkoro (1997) amebainisha sifa kuu ya mashujaa katika ngano za Zanzibar kuwa ni safari. Hivyo, Senkoro anaeleza kuwa shujaa ni lazima asafiri kutoka nyumbani kwenda kuishi mahali pengine. Senkoro anaeleza zaidi kuwa shujaa anaweza kusafiri kwa kufahamu au kutofahamu. Vilevile, Senkoro anaeleza kuwa safari ya shujaa inaweza kuwa ya masafa marefu ambayo itatumia muda mrefu au safari ya masafa mafupi ambayo itatumia muda mfupi. Hivyo, imebainika kuwa shujaa anaondoka nyumbani na kwenda kuishi sehemu nyingine kisha anarudi nyumbani. Katika Kisakale cha Munyigumba imebainika kuwa Munyigumba alisafiri kutoka Ng’uluhe kwenda kuishi Luhota kwa mjomba wake. Munyigumba alikwenda kuishi huko tangu akiwa kijana mdogo mara baada ya mama yake mzazi kufariki dunia. Hata hivyo, alipokuwa mkubwa shujaa huyo alirudi Ng’uluhe kuja kutawala baada ya kaka yake Ngawonalupembe kufariki dunia. Suala hili, limeelezwa katika kisakale hicho kama ifuatavyo:

...Baada ya msiba wa mama yake kuisha, Munyigumba aliamishwa na kwenda kulelewa kwa mjomba wake, Mzee Mihwela, huko Luhota...

Nukuu hii inadhihirisha kuwa shujaa Munyigumba aliamishwa kutoka nyumbani na kwenda kuishi uhamishoni ambako aliishi kwa muda mrefu mpaka alipokuwa kijana mkubwa.

4.11 Shujaa ni Rijali

Mbali na nduni hizo zilizokwisha kufafanuliwa, katika Kisakale cha Munyigumba imebainika kuwa shujaa ana nduni ya kuwa rijali. Nduni ya shujaa kuwa rijali inaendana na mawazo ya ki-Ontolojia ya Kiafrika, ambapo inaelezwa kuwa, Waafrika huthamini sana uzazi kwa sababu wanaona uzazi ndiyo njia ya uzima wa milele na ugumba ni laana mbaya zaidi kuliko laana zote (Chuachua, 2016; Mpalanzi, 2019). Aidha, wataalamu mbalimbali wanabainisha kuwa katika jamii za Kiafrika, suala la utajiri, mbali na kuhusishwa na mali alizonazo mtu, linahusishwa pia na idadi ya watoto na wake alionao mtu (Mulokozi, 2017; Sosoo, 2018). Hivyo, urijali ni suala muhimu sana katika jamii za Kiafrika, ikiwa ni pamoja na jamii za Wahehe. Suala la Waafrika kuthamini uzazi na shujaa kuwa rijali limesawiriwa katika kisakale cha “Munyigumba,” ambapo imebainika kuwa Munyigumba alikuwa rijali. Katika kisakale hicho, imeelezwa kuwa Munyigumba alioa wanawake watatu na alifanikiwa kupata jumla ya watoto kumi na mbili. Hii inaonesha kuwa shujaa huyu alikuwa rijali ambaye mke mmoja asingemtosha. Aidha, urijali huo ulimpatia watoto wengi tofauti na watu wengine ambao hawakuwa mashujaa katika jamii hii. Maelezo yafuatayo yanabainisha usawiri wa nduni hii katika kisakale teule.

...Mtawala huyo alioa wanawake watatu ambao ni Muyumbila Sengimba, Mulimwandi Semuvanga na Semutandamo Sengimba mdogo. Kwa kupitia wake zake aliowaoa, Munyigumba alibahatika kupata jumla ya watoto kumi na mbili...

Maelezo haya yanaonesha jinsi Munyigumba alivyokuwa rijali kwa sababu aliweza kuzaa watoto kutokana na wake zake alioawaoa.

4.12 Shujaa Huungwa Mkono na Wanajamii

Vilevile, nduni nyingine ya shujaa wa Kiafrika iliyobainika katika Kisakale cha Munyigumba ni shujaa kuungwa mkono na wanajamii. Nduni hii inaendana na Ontolojia ya Kiafrika kwani Waafrika huthamini sana umoja, mshikamano na ukamilishano wa maumbile na vilivyomo (Nicholaus, 2011; Mulokozi, 2017). Katika Kisakale cha Munyigumba, shujaa anaonekana kuungwa mkono na wanajamii, uungwaji mkono huu ndiyo unaomfanya shujaa kufanikiwa katika masuala mbalimbali. Aidha, uungwaji mkono huu unapokoma, unakuwa ndiyo mwanzo wa shujaa kuanguka na kufikia mwisho wake. Katika kisakale hicho imeelezwa kwamba shujaa Munyigumba anaonekana kuungwa mkono na watu

katika jamii yake. Wanajamii hao walikuwa tayari kumsaidia Munyigumba kupigana vita mbalimbali, ambavyo vilimfanya kutimiza azma yake ya kuwateka maadui zake na himaya jirani na hivyo kumfanya kuwa na nguvu nyingi za kivita, moja ya nduni za shujaa katika jamii hii. Kwanza, inasawiriwa kuwa Munyigumba alikuwa na jeshi kubwa ambalo aliongozana nalo hasa katika shughuli za kivita. Hii inabainisha wazi kuwa kama wanajamii wasingemuunga mkono Munyigumba, asingekuwa shujaa maana asingekuwa na nguvu za kivita. Usawiri huu wa shujaa kama mtu anayeungwa mkono katika kisakale husika unabainika katika maelezo yafuatayo:

...Munyigumba alikusanya vikosi vya kivita kutoka Luhota na akaamuru vikusanyike Rungemba. Munyigumba alipewa vikosi vingine na ndugu zake akina Kindole na hivyo akawa na jeshi kubwa kama utitiri. Munyigumba akaliongoza jeshi lake kuelekea Usangu kushambulia vijiji na kuteka wanawake na ng'ombe...

Hapa inabainika kuwa Munyigumba aliweza kuziteka jamii za jirani kutokana na kuwa na jeshi kubwa, jeshi ambalo wanajamii walikubali kumuunga mkono. Siku zote kwa Waafrika inabainika kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, umoja huo ndio ulimuwezesha Munyigumba kushinda katika vita alivyopigana na jamii mbalimbali ikiwamo Wangoni na Wasangu.

4.13 Shujaa Huogopwa na Wanajamii

Mbali na nduni hizo, pia shujaa Munyigumba alikuwa na nduni ya kuogopwa na wanajamii. Katika kisakale chake, imebainika kuwa kutokana na ushujaa wake, uhodari katika vita, nguvu zake za kimwili na nguvu zake za kisihiri, shujaa Munyigumba alikuwa anaogopwa sana na wanajamii. Hivyo, kinachobainika hapa ni kuwa wanajamii hawakuwa wanampenda shujaa huyo, bali walimwogopa kutokana na nguvu alizokuwa nazo. Kuogopwa huku kuliwafanya wanajamii kumtii na kutekeleza kila aliloagiza na hivyo alipata uungwaji mkono uliokitwa katika misingi ya woga na si mapenzi. Kwa mfano, katika Kisakale cha Munyigumba, imesawiriwa kuwa Munyigumba alikuwa anaogopwa na ndugu zake, Muyovela na Mwengamagoha, ambao waliamua kuikimbia nchi ya Uhehe. Kuhama kwa ndugu zake ambao walikuwa na maeneo yao waliyokuwa wanayatawala, kulimfanya Munyigumba kuongeza ukubwa wa himaya yake. Aidha, kwa kuwa ndugu hawa walikuwa na uwezo sawa na Munyigumba wa kuwa watawala, kuondoka kwao kuliendelea kumhakikishia Munyigumba kutawala kutokana na kukosa wapinzani. Hili linabainika katika maelezo yafuatayo kutoka katika kisakale husika.

...Munyigumba alikuwa ni mtu katili aungurumaye kama simba na wala haogopi mtu. Muungurumo wa Munyigumba uliwafukuzisha Muyovela na wafuasi wake wakaanzisha safari ya kuondoka Uhehe kuelekea Dodoma...

Kwa ujumla, imebainika kuwa shujaa Munyigumba alikuwa anaogopwa na wanajamii kutokana na mambo mbalimbali hasa ufundi wa kivita, umbile kubwa la kimwili na hata nguvu za kisihiri alizokuwa anazitumia.

4.14 Shujaa ni Mwanamume

Shujaa katika jamii ya Wahehe amesawiriwa katika Kisakale cha Munyigumba kuwa ni mwanamume. Suala la shujaa kuwa mwanamume katika jamii hii linaendana na Ontolojia ya Kiafrika kuwa katika jamii za Kiafrika, mwanamume hupewa hadhi ya juu kuliko mwanamke. Ni kutokana na hilo, katika jamii ya Wahehe, nduni ya ushujaa ilifungamanishwa na jinsi ya kiume na kwa namna yoyote ile, mwanamke asingeweza kuwa shujaa. Aidha, katika jamii hii, hata utawala ulionekana kuwa suala la wanaume, ambapo watoto wa kiume ndio waliorithi madaraka kutoka kwa wazazi wao. Ni kutokana na hayo, shujaa wao alikuwa mwanamume. Kwa mfano, katika Data Na. 12 usawiri wa shujaa Munyigumba kuwa ni mwanamume unabainika. Katika kisakale hicho, imeelezwa kuwa Munyigumba alikuwa ni mwanamume aliyeoa wanawake watatu na kupata jumla ya watoto kumi na mbili.

4.15 Shujaa Huhusishwa na zaidi ya Jamii Moja

Mbali na nduni zilizofafanuliwa, shujaa wa Kiafrika kuwa na nduni ya kuhusishwa na zaidi ya jamii moja imesawiriwa pia katika Kisakale cha Munyigumba. Shujaa Munyigumba alihusishwa na zaidi ya jamii moja kutokana na sababu mbalimbali. Kwanza, shujaa alikuwa anapenda kutawala eneo kubwa hivyo aliona kuwa kuna haja ya kutanua eneo la kumiliki. Pia, shujaa alihusishwa na zaidi ya jamii moja kutokana na mahusiano mazuri yaliyopo baina ya jamii moja na nyingine. Zaidi ya yote, suala la shujaa kuhusishwa na zaidi ya jamii moja linahusishwa na mhimili wa Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika unaosema kuwa Waafrika wanathamini umoja, mshikamano na ukamilishano wa maumbile na vilivyomo. Kutokana na hayo, inaaminika kuwa, Waafrika wanathamini maisha ya kuishi kwa umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii (Nicholaus, 2011; Samwel, 2015). Hivyo basi, katika Kisakale cha Munyigumba, imeelezwa kuwa Munyigumba alimua kiongozi wa jamii ya Wasangu aitwaye Munyigumba kisha akachukua madaraka ya kutawala eneo hilo (Data Na. 1). Vilevile, Munyigumba alitawala mpaka sehemu za Mufindi baada ya kumuua binamu yake Musambila kwa mkuki na akajitangaza yeye ndio mtawala mahali pale (Data Na. 7). Vilevile, Munyigumba alitawala Luhota baada ya kuwakimbiza watoto wa mjomba wake, Muyoveligombo na Mwengamagoha (Data Na. 14). Hivyo, kinachoonekana hapa ni kuwa Munyigumba anahusishwa na jamii ya Wahehe wa Ng'uluhe, anahusishwa na Wasangu na pia jamii za Luhota.

4.16 Shujaa Huvunja Miiko na Kanuni Zilizopo katika Jamii

Vilevile, usawiri wa nduni za shujaa katika Kisakale cha Munyigumba umebainisha kuwa shujaa katika jamii hiyo huvunja miiko na kanuni zilizopo katika jamii. Kitendo cha shujaa kuvunja miiko na kanuni za jamii ni cha Ontolojia ya Kiafrika kwa sababu shujaa anakuwa ameharibu dhana ya uduara wa maisha inayopatikana katika maisha ya Waafrika. Suala la shujaa wa jamii ya Wahehe kuvunja miiko na kanuni za jamii lilifafanuliwa katika Kisakale cha Munyigumba. Katika kisakale hicho, Munyigumba anavunja kanuni ya mtoto wa kiume wa mtawala kurithi madaraka. Hivyo, Munyigumba anamuua kaka yake, Ngawonalupembe, ili yeye ndiye awe mrithi wa utawala katika nchi ya Ng'uluhe (Data Na. 10). Kitendo hicho kinaonesha kuwa hakutaka kutii miiko na kanuni ya jamii ya mtoto wa kwanza kuwa mtawala na badala yake alitaka yeye awe mtawala.

4.17 Shujaa huwa na Majigambo

Shujaa kuwa na majigambo ni nduni nyingine ya shujaa inayosawiriwa katika Kisakale cha Munyigumba. Jamii ya Wahehe ni miongoni mwa jamii za Kiafrika zenye majigambo. Kitendo cha mashujaa kujigamba ni cha ki-Ontolojia ya Kiafrika kwa kuwa mashujaa huwa wanajigamba kufungamana na matukio maalumu katika maisha yao (Samwel, 2012; Mulokozi, 2017). Akifafanua mawazo hayo, Mulokozi (2017) anataja matukio maalumu ambayo shujaa anaweza kujifungamanisha nayo. Matukio hayo ni kama vile kuoa, kurejea kutoka vitani, kushinda jambo gumu kama vile kuua mnyama mkali au kushinda kesi mahakamani. Kwa mfano, katika Kisakale cha Munyigumba imebainika kuwa, Munyigumba alijigamba kuwa hakuna mtu anayeweza kumshinda katika vita baada ya kuokolewa na Mukwavinyika kutoka katika vita na Wangoni. Maelezo hayo yameelezwa katika kisakale hicho kama ifuatavyo:

...Baba wa Mukwavinyika, baada ya kuokolewa na mtoto wake katika vita na Wangoni, alifurahi na kurukaruka kama chura huku akijisifu kuwa hakuna mtu wa kumshinda katika vita. Mara tu baada ya kumaliza vita hivyo na Wangoni, Mukwavinyika alipewa jina hilo na baba yake kutokana na uhodari wake wa kivita....

Hivyo basi, kwa kawaida mashujaa wa Kiafrika hujigamba baada ya kushinda katika tukio fulani. Majigambo yalikuwa ni sehemu ya shujaa kujipongeza na kuioesha jamii kuwa yeye anaweza na hakuna jambo litakalomshinda. Hivyo, hata katika visakale vya jamii ya Wahehe, mashujaa walijigamba sana hasa baada ya kushinda katika vita.

4.18 Shujaa Hutoka Tabaka la Juu

Suala la shujaa kutoka katika tabaka la juu limejitokeza katika Kisakale cha Munyigumba, ambapo imebainika kuwa Munyigumba anatoka katika tabaka la juu kwa sababu alikuwa ni mtoto wa mtawala aitwaye Kilonge aliyetawala katika nchi

ya Ng'uluhe. Suala hili linabainika katika maelezo yafuatayo kutoka katika kisakale husika.

...Munyigumba alikuwa ni mtoto wa mtawala aliyetawala nchi ya Ng'uluhe aitwaye Mutwa Kilonge...

Mtawala Kilonge alipofariki utawala wa jamii ya Wahehe ulichukuliwa na mtoto wake mkubwa wa kiume aliyetwa Ngawonalupembe. Baada ya Ngawonalupembe kufariki dunia utawala ulibaki mikononi mwa Munyigumba. Hivyo, suala hii linaonesha dhana ya uduara wa maisha unaojibainisha katika mtindo wa kurithishana madaraka uliopo katika maisha ya Waafrika kama ilivyoelezwa na wafuasi wa Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika (Mulokozi, 2017; Mpalanzi, 2019).

5.0 Hitimisho

Makala hii imechunguza usawiri wa nduni za shujaa katika Kisakale cha Munyigumba wa jamii ya Wahehe. Kutokana na data zilizowasilishwa imebainika kuwa, nduni za shujaa zimejitokeza kwa namna mbalimbali katika kipera cha kisakale. Nduni hizo zimechambuliwa kupitia kipera cha kisakale kwa kuongozwa na mihimili ya Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Kutokana na hayo, imebainika kuwa, shujaa ana nduni zinazojumuisha nguvu za kivita, kisihiri, kiakili na kimwili. Nduni nyingine ni shujaa kuwa na umbo kubwa, shujaa kuwa na jina la heshima, shujaa kulipiza kisasi, shujaa kufuata kani ya nasaba ya kikeneni, shujaa kujumbia jaala yake, shujaa kusafiri kwenda kuishi uhamishoni, na shujaa kuwa rijali. Si hivyo tu, bali pia shujaa ana nduni ya kuungwa mkono na wanajamii, shujaa anaogopwa na wanajamii, shujaa ni mwanamume, shujaa anahusishwa na zaidi ya jamii moja, shujaa anavunja miiko na kanuni zilizopo kwenye jamii, shujaa ana majigambo na shujaa anatoka katika tabaka la juu.

Marejeleo

- Chuachua, R. (2016). Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Mustakabali wa Epistemolojia ya Kibantu. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Johnson, J. (1986). *The Epic of Son-Jara*. Bloomington: Indiana University Press.
- Kapinga, A. (2013). Dhima ya Nyimbo za Msiba katika Jamii ya Wahehe. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kezilahabi, E. (1985). *African Philosophy and the Problem of Literary Interpretation*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Wisconsin-Madison.
- Madumulla, J. (2017). *Proverbs and Sayings: Theory and Practice*. Dar es Salaam: TUKI.
- Malangalila, F.A. (1987). *Mwamuyinga: Mtawala wa Wahehe*. Peramiho: Benedict Publication.

- Mbiti, S.J. (1969). *African Religious and Philosophy*. Johannesburg: Heinemann Publisher.
- Mpalanzi, L. (2019). Ujitokezaji wa Falsafa ya Kiafrika katika Riwaya za Kiethnografia za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Msigala, D. (2015). Dhima ya Nyimbo katika Ngano za Jamii ya Wahehe. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mulokozi, M.M. (1988). *Mukwava wa Uhehe*. Dar es Salaam: DUP.
- Mulokozi, M.M. (1996). *Moto wa Mianzi*. Morogoro: ECOL Publication.
- Mulokozi, M.M. (2013). *Ngome ya Mianzi*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Mulokozi, M.M. (2018). *Ngoma ya Mianzi*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Ngassapa, D. (Mh.), (2011). *Mukwavinyika Mwamuyinga na Kabila lake la Wahehe*. Dar es Salaam: DUP.
- Nicholaus, A. (2011). Falsafa ya Ubuntu ilivyosawiriwa katika Tamthiliya Teule za Penina Muhando. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Ribeiro, O., Pimenta, S. na Moreira, F. (2019). "Nzinga Mbandi: From Story to Myth." *Science and Technology of the Arts*. 11: 51-59.
- Samwel, M. (2012). Mabadiliko katika Majigambo: Uchunguzi wa Majigambo ya Jadi na Bongo Fleva. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: MEVELI Publisher.
- Senkoro, F.E.M.K. (1997). The Significance of the Journey in Folk Tales from Zanzibar. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Sosoo, F. (2018). Ushujaa katika Motifu ya Safari na Msako: Ulinganishi wa Ngano za Kiewe kutoka Ghana na Riwaya za Shaaban Robert kutoka Tanzania. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Tempels, P. (1945). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine Publisher.